



Taarifa kwa Umma

UFAFANUZI: MITIHANI MAALUM NA MITIHANI YA MARUDIO HAIJAFUTWA

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimebaini taarifa zinazosambaa katika mitandao ya kijamii zikidai kuwa mitihani maalum na mitihani ya marudio imefutwa Chuoni. UDSM inapenda kuutaarifu umma, hususan wanafunzi, kwamba taarifa hizo si za kweli.

Mitihani maalum na mitihani ya marudio bado ipo na itaendelea kutolewa. Kilichobadilika ni wakati wa kuifanya. Ili kuongeza ufanisi wa kitaaluma mitihani hiyo sasa itafanyika ndani ya Kalenda ya kawaida ya kitaaluma ya Chuo. Mabadiliko haya hayaathiri viwango vya mitihani wala kubadilisha vigezo vya kuendelea na masomo.

Masharti mengine yote ya mitihani, yakiwemo masharti ya Wakia (GPA), hayajabadilika na yataendelea kutumika kwa mujibu wa kanuni za mitihani za Chuo zilizopo.

Wanafunzi wanakumbushwa kuzingatia masharti ya kozi zinazohitajika na kuwasiliana na vitengo vyao vya kitaaluma husika ili kupata mwongozo kuhusu hali zao za mitihani, upatikanaji wa kozi pamoja na taratibu za kukamilisha mitihani iliyosalia.

Chuo kinasisitiza umma kupuuza taarifa hizo za upotoshaji na kuzingatia kupata taarifa sahihi kupitia njia rasmi za mawasiliano za UDSM, ikiwemo tovuti ya Chuo (www.udsm.ac.tz), ili kupata taarifa sahihi.

Imetolewa na:

Prof. Rose A. Upor

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Taaluma

23 Oktoba, 2026